



YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI MASASI



TANGAZO

ZABUNI NA.LGA/135/2022/MTC/NC/07
KWA AJILI YA
KUKODISHA JENGO LA MEF NA ENEO LA WAZI MADEKO

MWALIKO WA ZABUNI

Tarehe: 10.07.2023

1. Serikali ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania kupitia **Halmashauri ya Mji Masasi** inakusudia kukodisha **jengo la MEF na eneo la wazi madeko.**
2. **Halmashauri ya Mji Masasi** sasa inakaribisha kampuni, Taasisi, kikundi na watu binafsi wenye uwezo wa kuomba zabuni za ukodishaji wa mali zilizo rodheshwa hapo chini.

SN	NAMBA YA ZABUNI	LOTI	MAELEZO
1	LGA/135/2023/2024/MTC/NC/07	1	Ukodishaji wa jengo la MEF
		2	Ukodishaji wa eneo la Madeko

3. Mwombaji anatakiwa awe na sifa kama zifuatazo;
 - i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea mwenye kitambulisho cha Taifa.
 - ii. Mwombaji aambatanishe nyaraka za kisheria kulingana na aina ya biashara/huduma anayokusudia kutoa yaani leseni ya biashara, Namba ya utambulisho wa mlipa kodi n.k

- iii. Kampuni/kikundi/Taasisi ziambatanishe hati ya nguvu ya kisheria (power of Attorney)
- iv. Mwombaji atataja aina ya biashara atakayoifanya na kodi ya pango anayokusudia kulipa kwa mwezi.
- v. Ada ya zabuni ni shilingi elfu 50,000.00 itakayolipwa kwa kutumia namba maalum ya malipo ya huduma (control number) zitakazopatikana **Halmashauri ya Mji, katika kitengo cha Fedha** (Gharama za ombi la zabuni hazitarejeshwa)
- vi. Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo,
Mkurugenzi,
Halmashauri ya Mji,
S.L.P 447,
Masasi.
- vii. Maombi yafungwe vizuri kwa bahasha yenye rakili kisha yawasilishwe kwa mkono katika **chumba Na.6, Ofisi ya mkuu wa kitengo cha ununuzi na ugavi, Halmashauri ya Mji Masasi, kabla ya tarehe 23.07.2023 saa 4.00 Asubuhi**
- viii. Waombaji wanaruhusiwa kufika katika ofisi ya Halmashauri ya Mji Masasi kwa ajili ya kukagua jengo na eneo lililokusudiwa kukodishwa katika siku masaa ya kazi kuanzia saa **1.30 Asubuhi** hadi saa **9.30 Alasiri (Jumatatu-ijumaa)**
- ix. Maombi yatakayochelewa,yatakayowasilishwa kwa njia ya posta/ barua pepe hayatapokelewa na hayatashughulukiwa.


Erica E.Yegella

Mkurugenzi wa Mji,
Masasi.